

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

SHULE YA SEKONDARI NAMBILANJE

S. L. P 03

RUANGWA.

TAR .....

Ndugu.....  
.....

**YAH; MAAGIZO YA MASHARTI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA  
SEKONDARI NAMBILANJE MWAKA 2021.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri katika mtihani wako wa Darasa la VII Mwaka 2020. Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika **Shule ya sekondari Nambilanje**.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ambazo unatakiwa kuzisoma kwa makini na kuzifanyia kazi.

- I. Fomu ya kupimwa Afya ya mwanafunzi kutoka kwenye Hospitali inayotambuliwa na serikali
- II. Fomu ya mahitaji muhimu ya shule
- III. Fomu ya sheria za shule
- IV. Fomu ya Taarifa za mwanafunzi na mzazi

Shule itafunguliwa **Tarehe 11/01/2021** siku ya **JUMATATU**. Nafasi yako itatunzwa kwa muda wa **WIKI MBILI TU**, tangu Tarehe ya kufungua shule. Hivyo unashauriwa kuwahi shule kabla nafasi yako haijazwa na mtu mwingine endapo utachelewa.

**MUHIMU:** Unatakiwa kuja na kivuli (PHOTOCOPY) ya **Cheti chako cha Kuzaliwa** (Nakala moja)

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya Maisha mapya ya shule ya sekondari .

**KARIBUNI SANA**

.....  
**LIBERATH THOMAS KINYAIYA**

**MKUU WA SHULE**

**0753 718 672**

## MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

1. SARE ZA SHULE (**WAVULANA**)
  - a. Wavulana wanatakiwa kuwa na suruali mbili(2) za **DARK BLUE** zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo
  - b. Mashati MEUPE mawili (2) yenye mikono mifupi na yenye kola shingoni.
  - c. Awe na sweta moja (1) rangi ya Bluu lililofumwa.
  - d. Viatu vya Ngozi (Vya kufunga na kamba) jozi (2), viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vyenye visigino virefu
  - e. Soksi imara nyeusi jozi mbili (2)
  - f. Nguo na viatu vya michezo (**FULANA NYEKUNDU NA BUKTA NYEKUNDU**)
  
2. SARE ZA SHULE (**WASICHANA**)
  - a. Wasichana watatakiwa kuwa na sketi mbili (2) za **KAROTI** zenye mshono wa **“Linda Box”**. Sketi iwe ndefu kupita magoti na ishonwe kwa unadhifu na sio kwa mapambo.
  - b. Mashati MEUPE mawili (2) yenye mikono mifupi na yenye kola shingoni.
  - c. Kwa wale wanaohitaji kuvaa **HIJAB** wavae Hijab nyeupe. Hijab isiwe ndefu kiasi cha kufunika mfuko wa shati.(Hijab isiwe na urembo wowote)
  - d. Awe na sweta moja (1) rangi ya Bluu lililofumwa
  - e. Viatu vyeusi vya Ngozi (Vya kufunga na kamba) jozi (2), viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vyenye visigino virefu.
  - f. Soksi imara nyeupe jozi mbili (2)
  - g. Nguo na viatu vya michezo (**TRACK SUIT NYEKUNDU**)

**MUHIMU:** Mwanafunzi ambaye atakuwa bado hajashona sare ya shule **ANARUHUSIWA** kuja shuleni akiwa na sare yake ya **Shule ya Msingi**. Mwanafunzi **haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani**.

Ili kuhakikisha kwamba sare zote zimeshonwa vizuri na kwa mlingano, usishone suruali au sketi bila kuja kupata maelekezo kutoka shuleni.

3. Fulana za shule zinapatikana shuleni kwa kununua
4. Vifaa vya usafi
  - a. Fagio mbili za chelewa
  - b. Jembe moja lenye mpini
  - c. Panga moja (Lililonolewa)
  - d. Reki moja
  - e. Ndoo ndogo moja
  - f. Fyekeo moja (Iliyonolewa)
  - g. Fagio laini la Dukani
  
5. Mahitaji kwa ajili ya Taaluma
  - a. Daftari 10 za quire mbili (2) au tatu (3)
  - b. Kalamu za wino wa bluu au mweusi na kalamu ya risasi (Penseli)
  - c. Mkebe 1 wa vifaa vya Hisabati (Mathematical Set)
  - d. Kamusi ya Kiingereza kwa kiingereza (English to English Dictionary) na kamusi ya Kiswahili kwa Kiswahili.
  - e. **REAM PAPER 1 (KARATASI RIMU 1)**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENTS' OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
RUANGWA DISTRICT COUNCIL

NAMBILANJE SEC. SCHOOL

P.O. BOX 03

**RUANGWA.**

REF. No..... DATE .....

THE MEDICAL OFFICER.

.....

.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF

.....

Please Examine the above named student and give us a regarding his/her suitability for secondary school studies.

1. Students' full name .....
2. Blood.....
3. Stool.....
4. T.B test .....
5. Syphilis test .....
6. Urine examination .....
7. Eye test .....
8. Chest .....
9. Ear .....
10. Spleen .....
11. Abdomen test .....
12. Pregnant test .....
13. OTHERS .....

I certify that the above student is **suitable/unsuitable** for studies

If unsuitable please give reasons.

.....  
.....  
.....

Name of medical officer .....

Signature of medical officer .....

Date .....

Official stamp .....

### **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inandeshwa kwa mujibu wa sharia ya elimu namba 25 ya Mwaka 1978. Aidha unatakiwa kuzingatia miongozo inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la **lazima**.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation) .
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi katika shule hii (Nambilanje secondary).
- (f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule .
- (g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (i) Wasichana **hawaruhusiwi kusuka nywele**.
- (j) Shule haimfungi mwanafunzi kuamini katika Imani yake ila kwa muda maalumu na siku maalumu.
- (k) Ajapo kuripoti aje na mzazi/mlezi. **Bila kuja na mzazi/mlezi hatapokelewa.**
- (l) Ni marufuku kuendesha ibaada wakati wa masomo.

### **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi, ugoro n.k
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya uma
7. Kudharau bendera ya taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza, au kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Mwanafunzi kuwa na **simu ya mkononi**
14. Mwanafunzi atakayekutwa anachafua kuta za shule atalazimika kulipa ndoo moja (01) ya rangi pamoja na Tsh. 20,000/= za ufundi ikiwa pamoja na adhabu nyingine atakayopewa.

**SHULE YA SEKONDARI NAMBILANJE**  
**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI NA TAARIFA ZA MZAZI NA**  
**MWANAFUNZI.**

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (kama kwenye mitihani yake) .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....
3. Kabila .....
4. Mahali na wilaya aliyozaliwa .....
5. Shule aliyomaliza darasa la saba .....
- Mwaka aliyomaliza .....
6. Dini .....
7. Michezo anayopendelea.

No	JINA LA MCHEZO
I	
II	
III	
IV	

8. Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile, kiranja, kiongozi wa kwaya, ngoma, michezo na kadharika.

No	UONGOZI	SHULE	MWAKA
I			
II			
III			
IV			

Nathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kamili na za kweli.

Nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe ..... sahihi .....

**SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI**

1. Jina kamili .....
2. Kabila .....
3. Dini .....
4. Mahali na wilaya anayoishi .....
5. Jina la Ndugu wa karibu na mwanafunzi .....
6. Namba ya simu ya mzazi/ mlezi wa mwanafunzi .....
7. Namba ya Ndugu wa karibu na mwanafunzi .....